NOVEMBA 2019 | NAMBA 25

# MAMBO MUHIMU

*Chapisho la kila Robo la Ofisi ya Tawi ya Ellen G. White - Adventist University of Africa*




## BIBLIA


*Mwongozo wa Imani Yetu*

Mamlaka ya Biblia 2

Mwenzi wa Kudumu 4

Unabii wa Biblia kwa Usomaji wa Leo 6

Makala ya Watoto 9




*Biblia ni kiwango ambacho kupitia kwacho mafundisho yote . . . ni lazima yapimwe*

# MAMLAKA YA BIBLIA

*Dondoo zimechukuliwa kutoka Ellen G. White Encyclopedia kurasa 645 - 647*

**P. Gerard Damsteegt**

Ellen White aliitambua Biblia kama ndiyo hasa Neno la Mungu, mafunuo makuu ya mapenzi yake, yasiyoweza kuanguka, kiwango cha imani na mazoea ya Kikristo yasiyoweza kukosea, na mamlaka ya juu kabisa kwa wanadamu. Kwa upande wake, mamlaka kuu ya Biblia imeweka mizizi yake katika madai yake kwamba Mungu ndiye mtunzi wake. "Biblia ni sauti ya Mungu inayosema nasi, kwa usahihi kiasi kwamba tunaisikia kwa masikio yetu" (*Testimonies for the Church*, volume 6, uk. 393). Biblia inafunua mapenzi ya Mungu. "Maandiko Matakatifu yanapaswa kupokelewa kama ufunuo wa mapenzi yake, wenye mamlaka na usioweza kuanguka" (*The Great Controversy*, uk. vii). "Mwanadamu anaweza kuanguka lakini Neno la Mungu haliwezi kuanguka" na ni "kiwango kisichoweza kukosea" (*Selected Messages*, book 1, uk. 416; *The Ministry of Healing*, uk. 462). Kwa hiyotunapaswa "kupokea Neno la Mungu kama mamlaka ya juu sana" (*Testimonies for the Church*, volume 6, uk. 402). Alikubaliana [EGW] na mwanamatengenezo wa Uingereza Wycliffe, aliyefundisha kwamba Biblia ni "mafunuo ya mapenzi ya Mungu yaliyovuviwa" na "kamilifu" (*The Great Controversy*, uk. 93). Mwishowe aliyakubali mamlaka ya Biblia bila uungwaji mkono wa malumbano mengine yaliyo nje ya Biblia. Kwa upande wake, "ushahidi wa ukweli wa Neno la Mungu, upo ndani ya Neno lenyewe (*Testimonies for the Church*, volume 8, uk. 157).

Biblia ndiye "mfunuaji wa mafundisho makuu ya Biblia," "kiwango ambacho kupitia kwacho mafundisho yote . . . ni lazima


yapimwe" (*The Great Controversy*, uk. vii). Ukristo wa kweli hulichukulia Neno la Mungu kama jumba kubwa la hazina ya ukweli uliovuviwa, na kipimo cha mafunuo yote" (*ibid*., 193). "Biblia, na Biblia pekee," alisisitiza, "ndiyo kanuni yetu ya imani" (*Counsels on Sabbath School Work*, uk. 84). Ipo haja kwa Wakristo kurejea kwa "kanuni kuu za Uprotestanti – Biblia, na Biblia pekee ndiyo iwe mwongozo wa imani yetu" (*Selected Messages*, book 1, uk. 416). Akionesha hisia kali katika imani kuwa Biblia ina mamlaka yake yenyewe katika mambo yahusuyo imani na mafundisho makuu, anasema: "Ningeweza kuruhusu mikono yangu yote miwili inyofolewe kutoka mabegani mwangu kuliko kutoa kauli au kutoa hukumu dhidi ya Neno la Mungu kuhusu nini kimevuviwa na nini hakijavuviwa . . . mwenye mwili wa kufa ye yote kamwe asithubutu kulihukumu Neno la Mungu" (*SDA Bible Commentary*, volume 7, uk. 919).

Ellen White aliweka mamlaka ya Maandiko juu ya mamlaka ya kitabu kingine chochote na kufundisha kwamba Biblia ndiyo chanzo pekee cha historia ya kweli ya kuaminika. Hata hivyo, alitambua kwamba, "kuelewa desturi za wale walioishi katika nyakati za Biblia" ni "elimu bora" ambayo "husaidia" kujifunza Biblia (*Counsels to Teachers*, *Parents*, *and Students*, uk. 518). Kuhusiana na usahihi na ukweli wake [Biblia] Ellen White anasema, "Ni hapa pekee tunapoweza kupata historia ya asili yetu isiyoharibiwa na mitazamo na majivuno ya kibinadamu" (*Patriarchs and Prophets*, uk. 596). Biblia hutuangazia umbali mrefu sana huko nyuma, ambako utafiti wa kibinadamu hutafuta kuupenya bila mafanikio. Ni katika Neno la Mungu pekee, tunapopata maelezo ya kuaminika kuhusu uumbaji" (*Testimonies for the Church*, volume 5, uk. 25). "Ni hapa pekee tunapopata maelezo ya kuaminika ya chimbuko la mataifa" (*Education*, uk. 173).

Alitoa maoni juu ya jitihada za kuhoji Biblia kwa kutumia sayansi: "Tena na tena wanadamu wamejaribu kuiweka Biblia na maandishi mengine ya wanadamu [wana sayansi] kwenye kiwango kimoja, lakini majaribio hayo yamethibitika kushindwa, kwa kuwa hatuwezi kumtumikia Mungu na mali" (*Fundamentals of Christian Education*, uk. 181). Ni "katika nuru ya ufunuo pekee" ambapo mafundisho ya vitu vya asili vinaweza "kusomwa sawa sawa" (*Education*, uk. 134).

Ellen White aliinua mamlaka ya Maandiko dhidi ya hekima, tabia, na uzoefu wa kibinadamu. Aliandika, "Werevu wa mwanadamu umekuwa ukitumika zama zote kupima Neno la Mungu kwa msaada wa akili zenye ukomo na uelewa wenye ukomo" (*Selected Messages*, book 1, uk. 18). "Lakini Neno la Bwana lisipimwe kwa viwango vya kibinadamu" (*Testimonies for the Church*, volume 5, uk. 301), na "filosofia haiwezi kuamua njia na kazi za Mungu; akili ya kibinadamu haiwezi kupima umilele" (*SDA Bible Commentary*, volume 6, uk. 1079). Anaonya kuwa, "Kipimo cha kibinadamu juu ya Mungu hakiwezi kamwe kuwa sahihi" (*Selected Messages*, book 3, uk. 308). Anaonya, "Maandiko hayapaswi kusomwa na mwanga hafifu wa tamaduni au dhana za kibinadamu. Kama tusivyoweza kujaribu kumulika jua kwa kutumia kurunzi, vivyo hivyo hatuwezi pia kuelezea Maandiko kwa kutumia tamaduni na dhana za kibinadamu" (*Christ's Object Lessons*, uk. 111). "Neno takatifu la Mungu halihitaji kumulikwa kwa mwanga wa kurunzi ya kidunia ili kufanya utukufu wake uwe bayana" kwa sababu "lenyewe ni nuru – utukufu wa Mungu uliofunuliwa, na ukiweka kando Biblia, nuru zingine zote ni hafifu" (*ibid*.).

Maandiko Matakatifu "ni kiwango cha tabia" na "kipimo ambacho . . . uzoefu wote unapaswa kupimwa" (*The Great Controversy*, uk. vii). Biblia ni "kipimo cha uzoefu na "kiungo pekee cha umoja" baina ya waumini (*ibid*.; *Selected Messages*, book 1, uk. 416).





# MWENZI WA KUDUMU

**Janet Oyende**

Ilikuwa ni mpaka nilipofikia umri wa utu uzima ambapo Biblia ilianza kuwa mwenza wa kudumu. Nilipokuwa nikihudhuria shule ya bweni ya elimu ya juu, ndipo nilipoanza kupata uzoefu wa uhalisia na nguvu ya Neno la Mungu. Fungu moja hasa liligusa akili yangu ya ujana wakati huo: "Mungu anatamani mtu afanyie mazoezi uwezo wake wa kufanya maamuzi; na usomaji wa Biblia utaimarisha na kuiinua akili kuliko masomo mengine yawezavyo kufanya" (*A Call to Stand Apart*, uk. 47). Hili linachochea kuwa na kiu binafsi ya usomaji wa Neno la Mungu.

Ilinichukua miaka kadhaa kujua namna ya kujisomea Biblia mimi mwenyewe na ni lazima nikiri kuwa bado ninaendelea kujifunza hilo. Nimegundua kuwa Biblia bado inahusiana na inafaa kutumika katika uzoefu wa maisha yangu ya kila siku. Hivi hapa ni vidokezo vichache vilivyonisaidia katika kujifunza Biblia, taa ya miguu yangu, Na mwanga wa njia yangu (Zaburi 119:105).

*Mungu anatamani mtu afanyie mazoezi uwezo wake wa kufanya maamuzi; na usomaji wa Biblia utaimarisha na kuiinua akili kuliko masomo mengine yawezavyo kufanya*

**1**

### Achana na Vitabu vya Hadithi za Kutunga

Maungamo ni mazuri kwa ajili ya roho. Lazima nikiri kwamba, nimevisoma vitabu vingi vya hadithi za kutunga na kuvifurahia sana. Hata hivyo, vitabu hivi vya hadithi vilikuwa vya uwongo na vya kushtua. Nilitambua kuwa kila baada ya kusoma vitabu hivi, vilifanya Biblia ionekane ya kuchosha na ya kuchukiza. Hivyo nikaacha kuvisoma vyote kabisa na Biblia ikawa ya kuvutia zaidi. (Soma *The Adventist Home*, uk. 412-414).

2

**Mtambue Anayeongea**

Masomo ya Biblia ni makutano baina ya akili ya Mungu isiyo na ukomo na akili yangu ya ukomo ya kibinadamu. Yule anayeongea kupitia Neno la Mungu ni Mungu Mwenyewe. Je, unaweza kupata picha ni maarifa na hekima ya kiasi gani ambayo Yupo tayari kukushirikisha?

3

**Omba**

Biblia ni ufunuo wa Mungu juu ya tabia yake kupitia kwa watakatifu wa Mungu kwa kadri walivyokuwa wakisukumwa na Roho Mtakatifu. Ni njia ipi iliyo bora zaidi ya kuisogelea Biblia zaidi ya kuomba uongozi wa Roho Mtakatifu kabla ya kuanza kukisoma? Omba na utapokea uelewa.

4

**Ifanye Tabia**

Kwa kadri nilivyodumisha masomo yangu ya Biblia ndivyo nilivyojisikia kuwa na hamu ya kuyahitaji zaidi. Nilipanga wakati na mahali maalum pa kufanyia masomo yangu ya Biblia, na matokeo yake, Biblia ikawa tamu kama asali (Zaburi 19:10). Kutokana na uzoefu wangu, niligundua kuwa nilitazamia sana kufika kwa wakati wa masoma yangu ya Biblia, niligundua kuwa ninaweza kujikumbusha masomo yaliyopita kwa urahisi, na huku nikiteua masomo na mada zinazofanana. Kadiri nilivyoyasoma, ndivyo nilivyoyapenda zaidi. Kadiri navyoyasoma, ndivyo utakavyoyapenda zaidi.

5

**Tumia Nguvu ya Ubunifu**

Kwa aya za Biblia zenye masimulizi, naweza kuweka kituo na kuanza kutafakari tukio. Hisia zote nitazikusanya pamoja [na kujiuliza]: mwandishi aliona nini? Alihisi nini? Aligusa nini? Alinusa nini? Alionja nini? Kwa kadiri nilivyohusisha hisia nyingi zaidi, ndivyo nilivyopata masomo mengi kutoka katika aya. Ilifanya Neno la Mungu kuwa halisi na lenye mguso.

6

**Kuweka Kumbukumbu**

Kila baada ya kusoma aya ya Biblia, ningeweza kuweka muhtasari wa mambo makuu niliyoyapata, kwenye kitabu cha kumbukumbu. Kuandika fungu kuu na vidokezo muhimu kuliimarisha somo akilini mwangu.

7

**Kutafuta Fursa za Kuwashirikisha Wengine**

Kwa kadiri nilivyosoma na Neno kuathiri moyo wangu, ningetafuta fursa za kushiriki lile Neno na wengine. Mara kwa mara ningeweza kuchukua fungu lililo kwenye aya lililonigusa zaidi na kulituma kupitia ujumbe mfupi wa maneno kwa watu wengi walio kwenye simu yangu kwa kadri nilivyoweza. Nilitiwa moyo wakati wengine wao walipojibu kuwa ulikuwa ni ujumbe uliokuja kwa wakati.

8

**Kutumia Fundisho**

Nguvu ya Neno la Mungu ipo katika kutambua kuwa linalo nguvu ya kugeuza na kubadilisha tabia na mazoea. Kila ahadi na amri imesheheni uwezo wa kufanya kile inachokisema.

Hebu uzoefu wako ukazidishwe na kuboreshwa kwa kadiri unavyokutana na Yesu kupitia kujifunza Biblia.

**Janet Oyende** anahudumu kama afisa wa mahusiano ya umma wa Adventist University of Africa, Nairobi, Kenya.



Upekee wa Biblia hautokani tu na waandishi wake bali unatokana na mtu inayemfunua.

# UNABII WA BIBLIA KWA USOMAJI WA LEO

**Brian K. Sinyangwe**

"Moyoni mwangu nimeliweka neno lako, nisije nikakutenda dhambi;" kwa kuwa "Neno lako ni taa yammiguu yangu, na mwanga wa njia yangu." (Zaburi 119:11; Zaburi 119:105). Katikammafungu haya, Daudi anathibitisha manufaa ya nguvu ya Maandiko katika maisha ya mwanadamu (Waebrania 4:12). Ellen G. White anazungumzia ukamilifu wa Maandiko katika mambo ya wokovu: "Biblia haikuandikwa kwa ajili ya msomi pekee; kinyume chake ilikusudiwa kwa watu wa kawaida. Ukweli mkuu ulio wa lazima kwa wokovu umefanywa wazi kama mchana kweupe; na hakuna atakayekosea na kupotea njia isipokuwa wale wanaofuata maamuzi yao wenyewe badala ya kufuata mapenzi ya Mungu yaliyofunuliwa wazi." (*Steps to Christ*, uk. 89).

Upekee wa Biblia hautokani tu na waandishi wake bali unatokana na mtu inayemfunua. Kuhusiana na Maandiko Yesu alifundisha; "Mwayachunguza maandiko, kwa sababu mnadhani kwamba ninyi mna uzima wa milele ndani yake; na hayo ndiyo yanayonishuhudia." (Yohana 5:39). Alijiweka [Yesu] yeye mwenyewe kama kiini cha ufunuo wake na muhtasari wa yote yanayoongelewa. Hii inaamsha hitaji kubwa la kujifunza kurasa zake.

Kipengele cha kuvutia kuhusu Biblia ni kwamba kimeundwa na vitabu sitini na sita tofauti tofauti vya aina mbalimbali za utunzi, jambo linalolazimu kuwepo kwa mwelekeo maalum wa namna ya kuvisoma. Aina mojawapo ya utunzi inayosumbua ni ile ya unabii. Ni aina ya utunzi ambayo baadhi ya wanafunzi wa Biblia,

wanatheolojia na hali kadhalika walei, hupata ugumu kuusoma na kuuelewa. Na hilo ni jambojingine linalowafanya wapoteze hamu ya kuchunguza kurasa zake.

Jukwaa la unabii wa kibiblia ni eneo la kuvutia linalowashughulisha wasomaji kuchunguza uhalisia wa wakati uliopita, uliopo, na ujao wa matukio ya kiulimwengu. Mandhari yake imesheheni mambo magumu ya kiungu na tafsiri za kiungu. Linaanza likionesha kana kwamba watu wa Mungu hawana tumaini na wanapoteza ushindi katika pambano la kilimwengu, lakini Mungu anayapindua matokeo yao ya vita na kuwa sherehe zenye utukufu.

### Migawanyiko Miwili ya Unabii

1. Mgawanyiko wa Kihistoria/Uliozoeleka: Hii ni aina ya unabii unaoshughulika na watu au matukio yanayohusiana na mwandishi kwa wakati alioandikia. Inajumuisha visa vyenye utajiri wa vifaa vya uandishi vinavyochora picha ya mtiririko wa kisa, eneo la tukio, na wahusika. Katika visa hivi, Mungu ndiye shujaa aliyeshinda. Unabii wa kihistoria kwa kawaida ni mrahisi kuuelewa kwa kuwa unawasilishwa kama matukio ya kihistoria na hivyo unapaswa kueleweka ndani ya uthamani wake na muktadha wake wa kihistoria.
2. Mgawanyo wa Kiapokaliptiki: Aina hii ya unabii inashughulikia kufunua masuala yanayohusu siku za usoni; mafunuo haya huambatana na njozi za masafa marefu kuhusiana na historia ya mataifa katika siku za usoni – na mara nyingi hulenga utawala wa kidunia. Kila tukio linalowasilishwa kwa namna moja au nyingine huunganishwa na tukio lingine lililotangulia na kile kijacho mbele kwa kawaida huwa ni ufafanuzi ama upanuzi wa kilichoelezewa awali. Jambo hili huhitaji ustahimilivu kidogo katika kutafuta tafsiri yake. Hata hivyo, Biblia inapaswa kuwa ndiyo mtafsiri wa awali katika unabii wa aina hiyo; ikizingatia lugha hiyo ya picha ilimaanisha nini katika nyakati na utamaduni za nabii huyo.

Katika baadhi ya vitabu vya unabii kama vile Danieli, migawanyiko inayotenganisha ufunuo wa kinabii ni wazi. Nusu ya kwanza ya kitabu hicho [Danieli] inawasilisha unabii uliozoeleka na ulio rasmi – ambao kwa sehemu kubwa ni ule wa kihistoria – yaani mambo yale yaliyotokea kwa watu halisi na katika nyakati alizoishi Danieli (Dan. 1 – 6). Nusu ya pili ya kitabu hicho (Dan. 7-12) inasughulikia unabii wa siku za mwisho – ambao kwa sehemu kubwa unachunguza matukio ya siku za mbeleni yanayovuka wakati anaoishi nabii (Dan. 12:8-9, 13). Hata hivyo, kuna muingiliano wa historia na unabii katika pande zote mbili za kitabu. Pamoja na hayo, umuhimu wa kila mgawanyiko unaonekana wazi.

### Uhusiano wa Maandiko ya Kiunabii Kwa Mwanafunzi wa Biblia wa leo

- Mungu pekee ndiye mwenye hekima: Katika jamii ya leo iliyovamiwa na wanaodai kuwa na huduma ya kinabii kutoka kwa Mungu, Biblia ndiyo sauti ya uhakika ya kiunabii ya kile Mungu anachofanya – (1 Tim. 1:17; Mith. 3:19; Isaya 55:9; Yoh. 12:13; War. 16:27). Wale wanaoweka tumaini na imani yao kwake hawatayumbishwa katikati ya machafuko ya maisha ya kisiasa, na kukosekana kwa uhakika kwa vitu vya asili na hali ya uchumi. Bado ni mwenye hekima hata katikati ya zahama (Isa 40:31). Imani isiyoyumba kwa ahadi zake ni lazima iende na walewanaojifunza Maandiko. Ahadi kama hizo zimetangazwa kwa wale wanaovutiwa na maandiko ya unabii (Uf.1:3). Kupitia maandiko ya kiunabii msomaji "hutambua kwamba Mungu hufanya kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia mema, yaani,wale walioitwa kwa kusudi lake" (Warumi 8:28).

*Kupitia maandiko ya kiunabii msomaji "hutambua kwamba Mungu hufanya kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia mema . . .*

- Mungu hujua siku za usoni: Maungamo ya wenye hekima wa Babeli (Dan. 2:11) yanakutana na majibu yao halisi kwenye uthibitisho wa Danieli mwenyewe kuhusiana na ufunuo huu (Dan. 2:28). Kristo anakiri hili katika mauaji ya mitume ya katikati ya karne ya kwanza (Uf. 1:8, 11, 17-18). Waumini wa leo wanapaswa kuamini kwamba Mungu anaujua wakati ujao. Kwa sababu anaujua wakati ujao, watakuwa salama watakapofungamanisha utii wao na makusudi yake. Hitaji lake kwa wanadamu siyo kuwadhuru bali kuwapatia mwisho mwema (Yer. 29:11).

- Mungu anaufunua wakati ujao: Mungu hafichi chochote kwa watu wake waaminifu. Huwafunulia siri zake (Amosi 3:7; Mwa. 18:17; Dan. 9:22; Yoh. 15:15). Ufunuo wa wakati ujao si vita dhidi ya ukweli uliokwisha kufunuliwa; badala yake daima huenda sambamba na ukweli mwingine wa Biblia. Kanisa la waliosalia [masalio] wa unabii wa Biblia linatambua kwamba mojawapo ya alama za kulitambulisha ni kumiliki na kudumisha Roho ya Unabii (Uf. 12:17; 19:10).
- Mungu humchagua wa kumfunulia yajayo (Math. 11:27; Luka 10:22): Ubinadamu hauna uwezo wa kuamua ni nani atakayefunuliwa na Mungu mapenzi yake na makusudi yake. Roho wa Mungu anaweza kumshukia yeyote kati ya mwanaume na mwanamke kwa kusudi la kufunua mapenzi yake kwa kuwa wanadamu wote ni wake (Yer. 32:27; Hes. 16:22; 27:16).
- Mungu bado anatawala haliya mambo: Kutambua kwamba Mungu bado angalianatawala hali ya mambo katikati ya hali isiyo ya kuaminika ya kibinadamu nijambo linalotujaza matumaini. Linatupatia uhakikisho kwamba licha ya vile mambo yanavyoonekana kuwa, mapenzi ya Mungu hatimaye yatashinda (Dan.1:1-2; 2:37;12:1-3; Isaya 42:12-13; Uf. 1:8, 17b-18; 22:7, 12). Hatima ya ubinadamu nahatima ya dunia iliyoumbwa, ile inayojulikana na ile isiyojulikana, vipo chiniya mkono unaotawala matukio wa Kristo. Licha ya kuwepo kwa vile vinavyoonekanakama vikwazo, bado Mungu ndiye mtawala wa mambo ya kesho kama alivyo mtawala wamambo ya leo. Kama kulikuwa nauhitaji wa kutumia muda katika kufanya uchambuzi wenye uangalifu wa Maandiko,basi mtindo wa uandishi wa kinabii unahitaji kupewa kipaumbele hicho. Ellen G. White anathibitisha "Tunaposogelea karibu na kufungwa kwa historia ya duniahii, unabii unahitaji kupewa kipaumbele chetu, kwa kuwa unahusiana sana nawakati tunaoishi." (*Prophets and Kings*, uk. 547).

**Brian K. Sinyangwe** ni mchungaji wa kanisa la Waadventista Wasabato anayehudumu katika konferensi ya Lusaka, Zambia. Hivi sasa ni mwanafunzi wa *MABTS - Systematic Theology* katika chuo cha Adventist University of Africa, Kenya. Yeye ni mumewe Mutinta na wamebarikiwa na mtoto wa kiume, Daniel.



# Makala ya Watoto

Robo hii tunajikumbusha jinsi Biblia ilivyo nzuri kwetu. Fanya bidii kukariri maandiko yafuatayo na kusoma Biblia yako kila siku.



*"Basi, kila anayesikiliza haya maneno yangu na kuyate keleza, atafanana na mtu mwenye busara aliyejenga nyumba yake kwenye mwamba."*
Matayo 7:24

*Kwa maana neno la Mungu ni hai tena lina nguvu; ni kali kuliko upanga wenye makali kuwili, linachoma kabisa na kutenganisha nafsi na roho, viungo vya mwili na mafuta yaliyomo ndani yake; na kutambua nia na mawazo ya mioyo ya watu.*
Waebrania 4:12

*Andiko zima lina pumzi ya Mungu nalo lafaa kwa mafundisho, kwa kuwaonya watu makosa yao, kuwaongoza na kuwafundisha katika haki.*
2 Timotheo 3:16

*Neno lako ni taa ya miguu yangu, Na mwanga wa njia yangu.*
Zaburi 119:105

*Mungu, njia yake ni kamilifu, Ahadi ya Bwana imehakikishwa, Yeye ndiye ngao yao. Wote wanaomkimbilia.*
Zaburi 18:30

*Jinsi gani kijana aisafishe njia yake? Kwa kutii, akifuata neno lako.*
Zaburi 119:9

*Basi muwe watendaji wa neno na wala msiwe wasikilizaji tu, ambao wanajidanganya wenyewe.*
Yakobo 1:22

*Hapo mwanzo, kabla ya kuwapo kitu kingine cho chote, alikuwapo Neno. Huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye alikuwa Mungu.*
Yohana 1:1

*Majani yakauka, au lanyauka; Bali neno la Mungu wetu litasimama milele.*
Isaya 40:8

Tutembelee kakika chuo kikuu cha
Adventist University of Africa Advent Hill,
Magadi Road, Ongata Rongai, Kenya

www.aua.ellenwhite.org
www.egwwritings.org

Ellen G. White Estate Branch Office - AUA

@egweboaua

Ili uweze kupata *Mambo Muhimu* kwa Kiingereza au Swahili, tuma ombi kwa
**egwebo@aua.ac.ke**
au utupigie simu
**+254-733-333-451/2**

**Ofisi za Utafiti za E. G. White Estate Barani Afrika**

**SID: Helderberg College**
Cape Town, South Africa
clarkec@hbc.ac.za

**ECD:University of Eastern Africa - Baraton**
Eldoret, Kenya
egwrc@ueab.ac.ke

**WAD: Babcock University**
Ilishan Remo, Ogun State, Nigeria
egwsdarc@babcock.edu.ng